

a ajili ya
ini, jijini

# hina

iwa Arusha Feb-
huu.
hilo, alisema pia
vitu mbalimbali
u viwili, nyundo
ya kuchorongea
Machine) moja
le tano mali za
u vingine wal-
yo gari aina ya
tumia kusafiria
a kwenda Dar es
namba za usajili
balo lilitelekezwa
ock Tower karibu
nki ya Exim, jijini
.
alisema baada ya
kamilika, jalada
fisi ya Mkurugenzi
(DPP) kwa hatua
ria.

# Serikali yageukia uvuvi maji asili

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali imeweka lengo la kuhakikisha sekta ya uvuvi kupitia ufugaji samaki inazalisha samaki wengi hasa wanaopatikana kwenye vyanzo vya maji vya asili.

Akizungumza jana alipokagua shughuli zinazofanywa na Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira mkoani Morogoro, Waziri Ndaki alisema sekta ya ufugaji samaki imekuwa na mwitikio mkubwa kwa sasa kutokana na mahitaji ya soko lake kuongezeka.

Alisema wizara itahakikisha inaendelea kuboresha miundombinu ya uzalishaji vifaranga vya samaki na kupanua zaidi wigo wa uzalishaji wake ili viende sambamba na mahitaji ya vifaranga kwa watu wanaofuga samaki.

Naye Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji kutoka wizara hiyo, Dk. Nazael Madalla, alisema wako katika hatua mbalimbali za kuendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa samaki ikiwamo kwa kutumia simu za mkononi.

Dk. Madalla alisema kupitia uboreshaji unaofanyika katika Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira, wako mbioni kuanza uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina Kambale.

Pia alisema kwa sasa vituo vya ukuzaji viumbe maji vilivyo chini ya wizara hiyo vimeanza kuza vifaranga aina ya sangara.

Kaimu Ofisa Mfawidhi wa Kituo hicho, Hamady Makorwa, alisema mkakati wao ni kuendeleza shughuli za uzalishaji ili kufikia lengo la kuzalisha vifaranga 600,000 kwa mwezi.

Alisema ili kufikia lengo hilo, kituo kinahitaji mabwawa 26 na samaki aina ya sato kwa ajili ya kuzalisha vifaranga 24,000 ambao kwa sasa wamefikia 5,430.

**TANGA FORESTS LIMITED**

The companies Act, 2002 (Section 334)

Scanned with CamScanner

# Soko la samaki wafugwao na maji ya asili kushindanishwa

**Na Edward Kondela**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema Serikali imeweka lengo la kuhakikisha Sekta ya Uvuvi kupitia ufugaji samaki inazalisha idadi kubwa ya samaki sambamba na samaki wapatikanao kwenye maji ya asili.

Akizungumza jana alipokuwa akikagua shughuli zinazofanywa na Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira kilichopo Mkoani Morogoro, Waziri Ndaki alisema tasnia ya ufugaji samaki imekuwa na mwitikio mkubwa kwa sasa kutokana na mahitaji ya soko la samaki kuongezeka hivyo jitihada nyingi zinafanyika kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki.

"Kwa sasa tasnia ya ufugaji samaki imekuwa ikitoa faida kubwa kwa wanaojishulisha na ufugaji hivyo natoa wito kwa watu kujitokeza kwa wingi kufuga samaki na pia na toa wito kwa vituo vyetu vya ukuzaji viumbe maji vilivyopo nchini kuhakikisha vinaongeza uzalishaji wa samaki kwa kuwa mahitaji ya vifaranga ni mengi." alisema Ndaki.

Aidha,alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi itahakikisha inaendelea kuviboresha vituo hivyo kwa kuboresha miundombinu ya uzalishaji vifaranga na kupanua uwezo wake ili viweze kwenda sambamba na mahitaji ya vifaranga kwa watu wanaofuga samaki.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt Nazael Madalla alisema wizara ipo katika hatua mbalimbali ya kupata programu maalum ya simu ya mkononi itakayoweza kutumiwa na watu wanaotaka kufahamu mambo mbalimbali kuhusu ufugaji samaki na namna ya kupata vifaranga vya samaki kutoka katika vituo ambavyo vipo chini ya wizara.

Pia, Dkt.Madalla alimfahamisha Waziri Ndaki uboreshaji ambao unafanyika katika Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira kwa kupanua shughuli za uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina ya sato na pia kituo kipo mbioni kuanza uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina kambale.

Kuhusu bei ya vifaranga vya samaki anasema kwa sasa vituo vya ukuzaji viumbe maji vilivyo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi vinauza kifaranga kimoja cha samaki aina ya sato kwa Sh. 100 na vimekuwa vikiwarahisishia wahitaji wa vifaranga kuwafikishia popote walipo bila ya ulazima wa wao kufika katika vituo hivyo.

Naye Kaimu Afisa Mfawidhi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Kingolwira Hamady Makorwa anasema mkakati ya kituo katika kuendeleza shughuli za uzalishaji ni kufikia uzalishaji wa vifaranga 600,000 kwa mwezi hivyo kituo kinahitaji mabwawa yasiyopungua 26 na sato wazazi wasiopungua 24,000 ambapo kwa sasa wapo 5,430.

Alifafanua kwa sasa vifaranga vya samaki vilivyopo katika kituo hicho ni 38,000 huku tayari wamepokea maombi ya vifaranga zaidi ya 180,000 kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alifika kwa mara ya kwanza katika Kituo cha Uzalishaji Viumbe Maji cha Kingolwira lengo likiwa ni kuhakikisha tasnia ya ufugaji samaki inakuwa kwa uwepo wa idadi kubwa ya upatikanaji wa vifaranga vya samaki nchini vitakavyouzwa kwa bei nafuu zaidi.

Mdiwani Sikonge wataka TFS kuweka utaratibu

kuhakikisha wanawake wanapata haki zao katika nyanja mbalimbali.

"Mmepambana sana kupinga ukatili wa kijinsia vikiwamo vitendo vya mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemevu wa ngozi na hata ubaguzi; kwa kweli Tamwa mme-

katika nafasi za uongozi na siasa kwa wanawake kwa kutumia taaluma yao," alisema Rose.

Mwenyekiti wa Tamwa, Joyce Shebe, alisema haki na usawa wa kijinsia ndiyo njia pekee ya kufikia maendeleo bila ubaguzi kwa watu wakiwamo watoto wenye ulemavu.

nchini kuanzia miaka 1964.

Tanganyika.

Profesa Silayo alisema

wamepanda asilimia 30 ya miti inayotakiwa kwa wakati huu.

## Tanga kuanza kugawa dawa za minyoo

**Na Amina Omari, Tanga**

ZAIDI ya wanafunzi 72,000 walioko katika shule za msingi katika Halimashauri ya Jiji la Tanga wanatarajiwa kupatiwa dawa za kukinga na kudhibiti magonjwa ya minyoo.

Hayo yamesemwa na Mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele katika Jiji hilo Dk Nassor Nassor wakati wa ugawaji wa dawa kwa watoto kuanzia umri wa miaka mitano katika shule za msingi 108 zilizoko katika jiji hilo zikiju-

muisha za serikali na binafsi.

"Niwaasihi walimu wahakikishe wanasimamia hilo zoezi la ugawaji wa dawa za minyoo kwa ukaribu ili liweze kutoa matokeo bora kama ambavyo walivyofanikisha ugawaji wa dawa za kichocho, matende na mabusha kwa

watu wazima" alisema Dk Nassor.

Alisema kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha wanadhibiti na kutokomeza magonjwa yasiyopewa kipaumbele ili yasiweze kuleta athari za ukuaji mzuri kwa watoto na kudhibiti kichaa.

# Ndaki aagiza uzalishaji zaidi wa vifaranga vya samaki

**Na Mwandishi Maalumu, Morogoro**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ameagiza vituo vya ukuzaji viumbe maji vilivyopo nchini kuhakikisha vinaongeza uzalishaji wa samaki kwa kuwa mahitaji ya vifaranga ni mengi.

"Kwa sasa tasnia ya ufugaji samaki imekuwa ikitoa faida kubwa kwa wanajishulisha na ufugaji hivyo natoa wito kwa wazalishaji vifaranga kuongeza kasi ya uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya soko," alisema Ndaki.

Waziri Ndaki alisema hayo juzi alipokuwa akikagua shughuli zinazofanywa na Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira kilichopo Mkoani Morogoro.

Alisema tasnia ya ufugaji samaki imekuwa na muitikio mkubwa kwa sasa kutokana na mahitaji ya soko la samaki kuongezeka hivyo jitihada nyingi zifanywe kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki.

Aidha, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi itahakikisha inaendelea kuviboresha vituo hivyo kwa kuboresha miundombinu ya uzalishaji vifaranga na kupanua uwezo wake ili viweze kwenda sambamba na mahitaji ya vifaranga kwa watu wanaofuga samaki.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Nazael Madalla alisema wizara ipo katika hatua mbalimbali za kupata programu maalum ya simu ya mkononi itakayoweza kutumiwa na watu wanaotaka kufahamu mambo mbalimbali kuhusu ufugaji samaki na namna ya kupata vifaranga.

Akizungumzia bei, Dk Madalla alisema kwa sasa vituo vya ukuzaji viumbe maji vilivyo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi vinauza kifaranga kimoja cha samaki aina ya sangara kwa Shilingi 100 na vimekuwa vikiwarahisishia wahitaji wa vifaranga kwa kuwafikishia popote walipo bila ya ulazima wa wao kufika katika vituo hivyo.

Naye Kaimu Afisa Mfawidhi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Kingolwira, Hamady Makorwa alisema mikakati ya kituo katika kuendeleza shughuli za uzalishaji ni kufikia uzalishaji wa vifaranga 600,000 kwa mwezi hivyo kituo kinahitaji mabwawa yasiyopungua 26 na sato wazazi wasiopungua 24,000 ambapo kwa sasa wapo 5,430.

Alifafanua kwa sasa vifaranga vya samaki vilivyopo katika kituo hicho ni 38,000 huku tayari wamepokea maombi ya vifaranga zaidi ya 180,000 kutoka maeneo mbalimbali nchini.

# Wafugaji nguruwe wataka kukatiwa bima

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFUGAJI wa nguruwe, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama Mjini, wameiomba serikali kuwaingiza kwenye mfumo wa bima za wanyama kama ilivyo kwenye vyombo vya moto, ili kuepuka na hasara ambayo wamekuwa wakiipata unapoingia ugonjwa wa homa ya nguruwe.

Mwisho mwa mwaka jana, uliingia ugonjwa huo, Wilaya ya Kahama na kusababisha nguruwe zaidi ya 500 katika mazizi matano ya wafugaji kufa na mwanzoni mwa mwaka huu, serikali ilisitisha biashara ya usafirishaji na uuzwaji wa nyama ya nguruwe mpaka tiba ilipopatikana.

Benny Mao, mwenyekiti wa kikundi cha Tujipambanue kaya ya Mwendakulima, aliyabainisha hayo juzi walipotembelewa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Patrobas Katambi, alisema, mwaka 2017 uliingia ugonjwa wa homa kali ya nguruwe kwa mara ya kwanza na kusababisha nguruwe wengi kufa.

Mao ambaye ni mwenyekiti wa wafugaji, alisema kama serikali ingewapatia bima za wanyama hao, wasingeendelea kupata hasara ya mifugo wanayopata, kwani wanawekeza fedha nyingi zinazopatikana na mikopo inayotolewa na halmashauri, lakini wanashindwa kuilipa kwa wakati hasa wakati wa ugonjwa huo.

"Kikundi chetu kina nguruwe 338 na asilimia kubwa ya fedha za uanzishaji wa mradihuuzinatokananamikopo inayotolewa na halmashauri yetu, mwanzo walitupatia shilingi milioni nane ambazo mpaka sasa tumesharejesha na tumeomba mkopo mwingine wa shilingi milioni 10," alisema Mao.

Aidha, alisema, gharama za uendeshaji wa mradi huo ni kubwa na kwa mwezi wanatakiwa kuwahudumia kwa chakula na madawa wanyama hao kwa kiasi cha Sh. milioni sita, lakini wanawahudumia Sh. milioni 3.8 matumizi ambayo hayakidhi mahitaji.

Naibu Waziri Katambi alisema bima hizo zipo na zinatolewa na serikali na taasisi binafsi ikiwamo taasisi za kifedha na zinasaidia kutoingia kwenye hasara linapotokea tatizo hasa unapoingia ugonjwa wa homa kali ya nguruwe.

Alisema bima ya mifugo inaweza kuwa inatolewa kwa gharama ndogo sana ukilinganisha na bima za magari na nyumba na kuwataka kuhakikisha kila mfugaji anakata bima za wanyama wake ili kuondokana na hasara ya kufa kwa mifugo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, alisema ugonjwa wa homa ya nguruwe uliingia na serikali ikaamua kusitisha biashara ya nyama na usafirishaji wa nyama hiyo, lakini kwa sasa biashara imefunguliwa, ila bado tunaendelea kuzuia katika Kata ya Kagonjwa.

TADB yatakiwa

Scanned with CamScanner

# Wizara kuboresha ufugaji samaki

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali imeweka lengo la kuhakikisha sekta ya uvuvi kupitia ufugaji samaki inazalisha idadi kubwa ya samaki hasa wanaopatikana kwenye vyanzo vya maji vya asili.

Akizungumza jana alipokagua shughuli zinazofanywa na Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira mkoani Morogoro, Waziri Ndaki alisema sekta ya ufugaji samaki imekuwa na mwitikio mkubwa kwa sasa kutokana na mahitaji ya soko lake kuongezeka.

Alisema wizara hiyo itahakikisha inaendelea kuboresha miundombinu ya uzalishaji vifaranga vya samaki na kupanua zaidi wigo wa uzalishaji wake ili viende sambamba na mahitaji ya vifaranga kwa watu wanaofuga samaki.

Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji wa Wizara hiyo, Dk. Nazael Madalla, alisema wapo katika hatua mbalimbali za kuendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa samaki ikiwamo kwa kutumia simu za mkononi.

Alisema kupitia uboreshaji unaofanyika katika Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira, wapo mbioni kuanza uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina Kambale.

Pia alisema vituo vya ukuzaji viumbe maji vilivyo chini ya Wizara ya hiyo Uvuvi vimeanza kuzaa vifaranga aina ya sangara.

Kaimu Ofisa Mfawidhi wa Kituo hicho, Hamady Makorwa, alisema mkakati wao ni kuendeleza shughuli za uzalishaji ili kufikia lengo la kuzalisha vifaranga 600,000 kwa mwezi.

Alisema ili kufikia lengo hilo, kituo kinahitaji mabwawa 26 na Samaki aina ya Sato kwa ajili ya kuzalisha vifaranga 24,000 ambao kwa sasa wapo 5,430.

